





7. Huduma zinazohusiana na afya

	<p>Upimaji wa macho</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ Mpimaji macho hushughulikia macho na uchunguzi wa kuona, kuidhinisha miwani na lenzi za plastiki na kutibu aina nyingi ya shida za macho ■ Mpimaji macho hafanyi upasuaji wa macho lakini anaweza kuidhinisha dawa ya kutibu maradhi ya macho ■ Wapimaji wengi wa macho hufanya kazi kibinafsi na wanaweza kupatikana katika vituo vingi vya ununuzi na maeneo raisi ya mitaa. Medicare hutoa usaidizi wa kupima macho mara moja kila miaka miwili isipokua kama kuna sababu za kliniki ambazo zinahitaji upimaji wa macho wa mara kwa mara. ■ Afya ya Queensland hutoa miwani ya bure kwa watu wanaostahiki kupitia Mpango wa Kutoa Miwani. Muulize mpimaji macho wako kama unastahiki mpango huu na jinsi ya kujiandikisha. ■ Shirika la Australia la Wapimaji macho www.optometrists.asn.au
	<p>Tibamaungo</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ Mtaalamu wa tibamaungo huchunguza, hubaini matatizo na kuwatibu watu walio na shida ya kutembea. Hao kwa ujumla huchunguza na kutibu viungo, misuli na majeraha ya mishipa ■ mtaalamu wa tibia maungo hutumia mbinu zinazo jumuisha: kukanda viungo, mazoezi na kunyoosa, usulihisho na utengenezaji wa viungo, mpakizi wa moto, barafu na uchunguzi wa viungo kupitia teknolojia mfano wa 'xray' isipokuwa inatumia sauti badili ya picha kwa kutazama viungo 'ultrasound'. ■ Katika huduma za umma, wataalamu wa tibamaungo hupatikana mahospitalini na vituo vya afya vya jamii. Utahitaji kuhakikisha kupitia hospitali yako ya mtaani au kituo cha afya ya jamii kama unastahiki kupokea matibabu kutoka kwa huduma hizi ■ Medicare husimamia katika baadhi ya huduma hizi chini ya Mpango wa Msingi wa Kuboresha maangalizi. Muulize daktari wako wa familia (GP) kuhusu huduma hizi. ■ Ukimuona mtaalamu wa tibamaungo kibinafsi, hauhitaji barua ya rufaa kutoka kwa daktari wako wa familia. ■ Shirika la Australia la Wataalamu wa Tibamaungo http://apa.advsol.com.au/physio_and_health/home.cfm
	<p>Utabibu wa vitengele vya mguu</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ wataalamu wa utabibu wa vitengele vya mguu hutoa ushauri juu ya afya ya mguu, kutathmini na kugundua shida/maradhi ya mguu, na kutibu shida za mguu ■ Wengi hufanya kazi kibinafsi na kwa hivyo lazima uwalipe moja kwa moja ■ Medicare husimamia katika baadhi ya huduma hizi chini ya Mpango wa Msingi wa Kuboresha maangalizi. Muulize daktari wako wa familia (GP) kuhusu huduma hizi. ■ katika huduma za afya ya umma wanahusika na kupima ugonjwa wa sukari na huduma ya miguu; huduma ya vidonda; kliniki za mishipa ya damu na kazi zingine. ■ Baraza la Waustralia la Utabibu wa vitengele vya mguu www.apodc.com.au/index.shtml
	<p>Saikolojia</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ Wanasaikolojia huwasaidia watu kupunguza shida na kuboresha maslahi ya mhemeko ■ Wanaweza kuwasaidia watu ambao wana mhali wa kudhibiti hisia, mafikiria na tabia zao. ■ Wengi hufanya kazi kibinafsi na kwa hivyo lazima uwalipe moja kwa moja ■ Medicare husimamia katika baadhi ya huduma hizi chini ya Mpango wa Msingi wa Kuboresha maangalizi. Muulize daktari wako wa familia (GP) kuhusu huduma hizi ■ Shirika la Saikolojia la Australia www.psychology.org.au